

JE DOCS INASAIIDIA FAMILIA?



KUHIFADHI WATOTO NA KUUNGA FAMILIA

DoCS inamaanisha Wizara ya Huduma za Jumua ya NSW (NSW Department of Community Services).

Kazi yetu muhimu ni kuhifadhi watoto. DoCS inasaidia familia kwa kulea watoto na vijana wenye furaha, nguvu na afya njema.

Watoto ni wa thamani na sisi wote tunataka maisha bora kwa watoto wetu. Lakini familia nyingi zinahitaji msaada na fadhila ili zitunze watoto.

Familia mbalimbali zina matatizo zaidi yanayofanya maisha yawe magumu, kama:

- Hakuna ndugu au marafiki wanaoishi karibu ili wawapatie msaada
- Ukosefu wa kazi, maradhi, upekee au upweke
- Uzoefu usiotosha katika mambo ya uzazi
- Matatizo yanayotokana na kileo na dawa za kulevya
- Vurugu za nyumbani

DoCS inasaidia familia zinazohitaji msaada.

JE DOCS INASAIIDIA FAMILIA?

Kuwa mzazi kunaweza kuwa tatizo kubwa. Hivyo, msaada na fadhila kuweza kubadili hali ya mambo.

DoCS inatoa fedha kwa shirika zinazosaidia familia katika huduma tofauti kama kuzuru nyumbani, azimio ya uzazi na vikundi vya michezo.

Miradi kama *Families NSW* na *Brighter Futures* yanaleta msaada kwa familia kupitia huduma kama kuzuru nyumba, azimio ya uzazi na vikundi vya michezo.

Miradi hii inajenga familia na jumua imara ili kupanga maisha bora ya watoto na vijana

Kazi yetu kubwa ni kuhifadhi watoto na vijana katika NSW kutokana na mateso na upuuzi – hii inaitwa ulinzi wa watoto

DoCS inashirikiana na shirika nyingine za serikali na vyama vya jumua katika ulinzi wa watoto.

KUNA UHUSIANO KATI YA SHERIA NA FAMILIA?

Kama wazazi tunawajibika kulinda watoto wetu lakini mara nyingine familia hazina uwezo wa kufadhili na kutunza watoto wao.

Sheria zinazohusu ulinzi wa watoto zimetungwa kwa ajili ya kuhifadhi watoto wote na vijana wenye umri chini ya 18.

Sheria inakataza kuumiza, kudhuru, kutesa au kupuuza watoto.

Upuuzi ni wakati wazazi hawahudumii mahitaji ya msingi ya mtoto kama mahali pa kulala, chakula, mavazi na matibabu ya afya.

Mateso ya kimwili ni wakati mzazi anaumiza mtoto kwa kumgonga, kumpiga, kumtukusa, kumchoma au kwa namna nyingine.

Mateso kuhusu mhemuko yanaweza kuwa ukosefu wa mapenzi, kutisha, kudhulumu au kutia watoto katika vurugu za nyumbani.

Mateso ya kijinsia ni kuingiliana na watoto kwa namna yeyote.

KWA NINI DOCS INAHUSIKA NA FAMILIA?

DoCS inashirikiana na familia kwa kuzisaidia kubakia pamoja na kutunza watoto wao.

DoCS ina wajibu wa kutunza na kulinda watoto na vijana katika NSW.

Simu ya kusaidia ya DoCS kupokea ripoti nyingi kuhusu watoto wenye hatari ya kuteseka na kupuuzwa. DoCS kushirikiana na familia ili kuhakikisha kuwa watoto wako salama.

Wakati mtoto hana usalama katika familia yake, DoCS inaweza kutafuta familia salama ya ndugu au mlezi. Hii inaweza kuwa kwa mda mfupi au mrefu.

DoCS haitachukua nafasi ya familia au jumua katika ulezi wa watoto.

NANI ANAWEZA KUSAIDIA?

Simu ya Wazazi (saa 24)	132 055
Huduma za Habari kwa Familia	1800 049 956
Simu ya Kusaidia ya Wazazi wa Tresillian	1800 637 357 (02) 9787 0855 (Sydney)
Simu ya Kusaidia Watoto	1800 551 800
Simu kuhusu Vurugu za Nyumbani	1800 656 463
Huduma za Tafsiri na Ufananzi	131 450
Simu ya Kusaidia ya DoCS	132 111
Kwa ajili ya malalamiko kuhusu ya DoCS	Simu sabili 1800 000 164

Habari kuhusu huduma za familia zinapatikana kwenye:
www.community.nsw.gov.au
www.families.nsw.gov.au
www.raisingchildren.net.au



NSW Department of
Community Services